

# Ukweli wa Injili

MAFUNDISHO YA BIBLIA NA HIMIZO KWA  
KAZI YA KIMISHENI ULMWENGUNI KOTE


## KUTOKA BABELI HADI PENTEKOSTE AU “KUONGEA KWA LUGHA NYINGINE”

“Bwana....(akasema) Haya, na tushuke huko, tuwachafulie usemi wao ili wasisikilizane maneno wao kwa wao....Kwa sababu hiyo jina lake likaitwa Babeli” (Mwanzo 11:6-9).

Baada ya gharika ile kubwa ambayo ilitokea wakati wa Nuhu, watu walanza (tena) kuwa waovu mbele zake Mungu. Kwa kiburi chao cha moyo wakaanza kujenga mnara ili kufika mbinguni, mnara ambaao ulijulikana kama “Babeli.” Na katika kukatisha kiburi chao cha wao kuabudu sanamu Mungu aliwafanya kuanza kunena kwa lugha tofauti tofauti. Mbeleni ulimwenguni “Nchi (dunia) yote ilikuwa na lugha moja na usemi mmoja” (Mwanzo 11:1). Basi kwa kukosa lugha moja umoja wa watu hao haungeendelea, na wakatawanyika kote ulimwenguni. Basi hapa ndicho chanzo cha lugha tofauti tofauti ulimwenguni.

Baada ya miaka 2000 hivi katika siku hiyo ya Pentekoste wafuasi 120 wa Yesu walikuwa kwenye chumba hicho cha juu wakimtafuta Baba kwa umoja, “Kukaja ghafula toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi....Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka” (Matendo 2:2-4).

Kikundi kikubwa cha watu ambacho kilihusisha Wayahudi kutoka kwa kila taifa ulimwenguni kilikuja pamoja ili kushuhudia ishara hii ya kimuujiza. Na kwa sababu wengine hawakuelewa kilichokuwa kikiendelea wengine wao



*Hapo Babeli lugha ziligawanya watu.  
Hapo Pentekoste watu wakapata umoja  
kupitia kipawa cha kimuujiza cha lugha  
ili Injili ielewewe.*

wakasema kwamba wanafunzi hao walikuwa wamelewa pombe. Lakini Mungu alikuwa amemwaga Roho wake kati ya waumini wa Yesu Kristo nao wakashuhudia Injili kupitia kwa ishara na mambo mengine ya kiajabu, huku wanafunzi hao wakinena kwa “lugha nyingine.”

Katika ulimwengu wa kidini kuna mambo mengi ambayo yanasemwaa kuhusiana na “kunena kwa lugha nyingine” kama ilivyofanyika katika siku ya Pentekoste. Je, kwa kweli ni nini kilitenda siku hiyo? Je, wanafunzi hawa walikuwa wakinena kwa njia gani? Je, hizi “lugha nyingine” zilikuwa za kiroho, za kibingu, au za kimalaika? Hakuna haja ya kuwachia wanathiolojia au ujuzi wa kihisia wa mtu binafsi ili kuelezea ukweli kuhusu kipawa cha kunena kwa lugha nyingine. Neno la Mungu linadhahirisha uhalisi na ukweli wa kipawa hiki.

“Basi sauti hii iliposikiwa makutano walikutanika, wakashikwa na fadhaa, kwa kuwa kila mmoja aliwasikia wakisema kwa lugha yake mwenyewe” (Matendo 2:6). Jambo hili ni rahisi na dhahili kabisa. Wanafunzi hawa hawakuwa wakisema kwa njia isioleweka kwa kutumia lugha ya malaika yenye kuwalettea furaha moyoni. Watu hawa wa Galilaya (ambao wengi wao walikuwa ni wavua samaki wasiokuwa na elimu kubwa) walikuwa wakinena kwa kutumia lugha zaidi ya 12 za watu ambaao walikuwa wamekusanyika hapo: “Imekuwaje basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu tuliyozaliwa nayo?” (Matendo (Inaendelea kutoka ukurasa 2)

# MAMBO AMBAYO

# BIBLIA

## Inafundisha Kuhusu...

### Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

### Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, I Yoh. 4:7-21

### Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

### Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6

### Uhuru Kutokana na Dhambi

I Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

### Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

### Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, I Pet. 1:15-16,

Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

### Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

### Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, I Kor. 12:12-13,

Kol. 1:18

### Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

### Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,

Yn. 13:14-17

### Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

### Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3,

I Kor. 7:10-11

### Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

### Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt.

25:31-46

### Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

### Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

(Endelea kutoka ukurasa 1)

2:8). Watu kutoka bara Asia na Afrika na hata toka mji wa Roma (Matendo 2:9-11) walishangaa na kupigwa na butwa walipokuwa wakisikiliza wanafunzi hawa.

Wanafunzi hao hawakuwa wamejifunza lugha hizi; lakini kwa jinsi ambavyo Roho Mtakatifu aliwapatia uwezo wao waliweza kuwasiliana kwa lugha ya kigeni ili watu kutoka nchi zingine waweze kuelewa. Walikuwa wakitabiri au kuhubiri kuhusu Yesu Kristo Mwana wa Mungu aliye hai: "Tunawasikia hawa wakisema kwa lugha zetu matendo makuu ya Mungu" (Matendo 2:11b). Kipawa hiki kilikuwa kimetolewa kwa wanenaji, na sio kwa wasikilizaji wao. Kwa mfano, huenda Petro alikuwa akihubiria kikundi kimoja kwa lugha moja ya Asia. Na kwa upande mwingine huenda naye Yohana alikuwa akiwhubiria watu hao kwa lugha ya Kiarabu, n.k.

Watu wa Babeli waligawanyika kwa sababu ya wao kuchanganyikiwa kutokana na kila mtu kunena lugha tofauti. Lakini katika siku ya Pentekoste wote waliweza kusikia ujumbe wa Yesu Kristo, wenye kuleta umaja, kwa njia ile ya kipawa cha kiungu cha kunena kwa lugha zingine. Ingalkuwa kwamba wanafunzi hao walikuwa wakitoa maneno yasioeleweka au vilio kutoka ndani mwao kama jinsi ambavyo watu wa siku hizi ambaudhudia kwamba "wananena kwa lugha zingine" hufanya basi wasikilizaji wao wangebaki wakiwa wamechanganyikiwa. Lakini, kama ambavyo ilikuwa watu kutoka mataifa yote walisikia ujumbe wa wokovu kwa lugha zao za mama.

Basi sisi tunamshukuru Bwana wetu Yesu ambaye ndiye aliwawezesha wanafunzi hao kuwashuhudia watu hao wa kigeni kwa njia ya Roho Mtakatifu kwa lugha za kwa wenye: kutoka Babeli hadi Pentekoste, kutoka magawanyiko hadi umaja, kutoka hali ya kuchanganyikiwa hadi kufikia hali ya kueleweka, kutoka kwa hali ya dhambi hadi kufikia wokovu.

—mws

### UKWELI WA INJILI

Gazeti la 'Ukweli wa Injili' huchapishwa kwa jina la Bwana kwa matumizi ya watu wa mataifa yote kwa kusudi la kuimaraisha na kuwahimiza watu wote katika ukweli wa neno la Mungu. Gazeti hili hufundisha na kueneza ukweli wa Biblia ambaudhudia tangu nyakati ya Yesu Kristo na mitume. Neno la Mungu ndio mwongozo halisi na wa kipekee wa imani. Linafundisha wokovu na ukombozi kutokana na dhambi unaotewa na utakaso wa Yesu Kristo; ambaudhudia tangu nyakati ya Roho Mtakatifu anayemwongoza mhudumu, kumwonyesha njia, na kumpatia nguvu; pia unamletea mtu utakatifu halisi katika kila fani ya maisha yake; na pia kuleta umaja na utangamano wa watu wa Mungu. Huduma inayokubalika na Mungu inatokana na mtu kuwa na uhusiano wa kibinagsi na wa upendo ambaudhudia msingi wake ni ukweli.

Waandishi: Michael na René Smith

### UAGIZAJI

*Ukweli wa Injili* ni gazeti la kieletroniki linalochapishwa kila robo ya mwaka kwa jinsi mungu anavyotuongoza. Tutembelee katika tovuti yetu ya [www.thegospeltruth.org](http://www.thegospeltruth.org) ili uagize jalida hili kuptitua kwa orodha yetu ya anwani pepe na upokee toleo lako la wakati huu. Hebu jisikie huru kututumia orodha ya majina na anwani pepe za watu wengine ambaudhudia tangu nyakati ya Roho Mtakatifu anayemwongoza mhudumu, kumwonyesha njia, na kumpatia nguvu; pia unamletea mtu utakatifu halisi katika kila fani ya maisha yake; na pia kuleta umaja na utangamano wa watu wa Mungu. Huduma inayokubalika na Mungu inatokana na mtu kuwa na uhusiano wa kibinagsi na wa upendo ambaudhudia msingi wake ni ukweli.

### WASILIANA NASI

Gazeti a *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika mataifa mbalimbali ili kusambazwa katika maeneo hayo. Kazi hii na zingine za kimishenari ambazo sisi hufanya huwezekana kuptitua kwa matoleo ya kujitolea yanayotolewa kwa jina la Kanisa la Mungu.

# Tahariri



*Ndipo Petro, akijaa Roho Mtakatifu, akawaambia...." —Matendo 4:8.*

Akiwa amejaah Roho Mtakatifu Mtume Petro hakuanguka chini, pia hakuanza kutetemeka na kupepesuka, hakuanza pia kuropokwa, hakuanza kutokwa na pofu la mate mdomoni; badala yake Petro alinena kwa ujasiri, kwa uwazi, na kwa nguvu za imani kuhusu Bwana ambaye alishafufuka. Je, ni baraka ya ajabu kiasi gani mtu kuwa na ujuzi na uhalisi wa ubatizo wa Roho Mtakatifu ambao ndio hutupatia nguvu na kutuwezesha kuishi maisha matakatifu!

Katika toleo hili la *Ukweli wa Injili* mimi nitanena kuhusu unenaji kwa lugha nyingine. Hili ni somo kubwa sana na ni la muhimu sana hivi kwamba nimeongezea kurasa za gazeti hili. Lakini hata ingawa nimeongezea kurasa hizo kuna mengi zaidi ambayo yanaweza kuandikwa kuhusu swala hili. Biblia iko dhahiri kabisa kuhusu kile ambacho kilitendeka siku hiyo ya Pentekoste wakati ambapo wanafunzi walinenia kwa lugha zingine. Watu hao walipata uwezo wa kuhubiri kwa lugha ambazo zilieleweka, ambazo hapo mbeleni hawakuzijua, kupitia kwa kipawa cha kiungu kilichotokana na Roho Mtakatifu. Shetani amepotosha urahisi wa ujuzi hii na kuhadaa mamilioni ya watu hata wakaanza kufikiria kwamba kuna lugha ya mbinguni, na kwamba kunena au kuomba kwa furaha ya moyo kwa kutumia lugha isioeleweka ni jambo ambalo linatokana na Roho Mtakatifu.

Kwa kweli usemajii kwa lugha sisioeleweka ni jambo ambalo haliko tu kwa dini za Kipentekoste, linapatikana pia kati ya dini zote za kidunia na dhehebu zote za Kikristo. Bila hofu yoyote na bila kusitasita mimi natangaza katika Bwana Yesu kwamba roho huyu wa kunena maneno yasioeleweka hatokani na Roho Mtakatifu; ni roho ambaye ni kinyume na mazoea na mafundisho ya roho ambaye anapatikana katika Kristo na katika Neno lake. Lakini kwa maneno hayo wengine watanikashifu na kusema kwamba mimi namtusi Roho Mtakatifu. Na kwa kweli tayari nishapata lawama hizo lakini mimi nasimama na mwanga wa Neno la Mungu na pia kulingana na jinsi mimi binafsi nimefunuliwa ukweli huo.

Tayari nishakutana na roho na mazoea ya watu kunena lugha sisioeleweka sio tu hapa Marekani bali pia hata kwenye mataifa mengine mengi. Wakati nafundisha wahudumu kutoka madhehebu tofauti tofauti hakuna somo ambalo humkasirisha Shetani kama hilo la uneni kwa ndimi nyingine. Basi ni muhimu kabisa kwamba tunahitaji kufuata mfano wa Yesu kuhusiana na maswala ya maombi na hata kitabia.

Madhehebu mengi yamechukua "msimamo usioegemea upande wowote" kuhusiana na swala hili la kipagani la kuomba au kunena kwa maneno yasioeleweka. Lakini jinsi watu wanajaribu kukosa kuhukumu jambo hili, ndivyo milango hufunguka kwa mafundisho mengine ya uwongo, na pia kuingia kwa roho ambazo hazitokani na Mungu. Basi hata tukisema kwamba chanzo cha roho huyu ni hisia za kibinadamu, au maswala yanayomzunguka mwanadamu, au kwamba inatokana na roho sisizo za kweli, ukweli ni kwamba, roho huyu wa kunena mambo yasioeleweka hutokana na Shetani na kusudu lake ni kuwahadaa wanadamu.

Ni jambo la kushangaza kwamba kuna dini za kipagani na za watu ambao hawaamini Mungu ambazo washirika wake pia huwa na ujuzi huu unaolingana na ujuzi wa washirika wa madhehebu ya Kipentekoste na hata dhehebu zingine ambao wao wanadai kwamba ni dhihirisho la uwepo wa Roho Mtakatifu. Wengi wa washirika hao wa vikundi vyta kipagani huwa wanaishi dhambini lakini wao hujidai kuwa watu wa kiroho kwa sababu wana ujuzi huo wa kunena kwa lugha nyingine.

Mimi ninaamini kwamba hii ni mojawapo ya njia kubwa ambayo adui hutumia kuwahadaa Wakristo katika ulimwengu wa kisasa. Basi hebu tuwe watu wa maombi na daima tuwe macho dhidi ya adui wetu Shetani. Tunaomba kwamba Mungu ataangazia macho yetu yenye giza ili tupate kuona.

Michael W. Smith

Julai 2014


mengi kwa  
MTANDAO

**Tutembelee kwa**

[www.thegospeltruth.org](http://www.thegospeltruth.org)

**ili uagize na kusoma**

**jarida letu.**



# KWA LUGHA YA KIYUNANI

## Dialektos (Dee-AHL-ek-toss)

Kulingana na *Kamusi ya lugha ya Kiyunani ya Strong*: (njia ya) kuwasiliana, maanake “lahaja”: lugha, ndimi.

**Glossa** (GLOSS-uh) Neno la Kiyunani lenye maana ya “ndimi” ama “lugha.”

*Mpangilie wa Maneno ya Kiyunani kwenye kitabu cha Thayer: Glossa:* 1. Ndimi, sehemu ya mwili, kiungo cha uneni. 2. Ndimi, lugha inayotumiwa na watu fulani tofauti na lugha inayotumiwa na watu wa mataifa mengine.

**Kwa kusudi la toleo hili neno glossolalia limetumika kuzungumzia tabia ya watu kunena maneno ambayo hayaeleweki, kwa lugha ambayo haijawahi kuweko (maanake uneni usioeleweka).**

## Glossolalia (GLOSS-uh-LAY-lee-uh)

Neno hili limetokana na maneno mawili ya Kiyunani: *glossa* (maanake lugha au ndimi) na *lalia* (manake kuongea ama hotuba). Kwa maana yake halisi neno hili linaweza kumaanisha mtu kuongea kwa lugha za kigeni. Lakini katika siku zetu neno hili linatumiwa na wanathiolojia kuzungumzia mazoea ya kunena au kuomba kwa kile ambacho kinajulikana kama lugha ya mbinguni au lugha ya kiroho (mtu kutoa maneno yanayomletea uchungamfu moyoni kulingana na jinsi inavyotumiwa katika dini za kisasa ambazo washirika wake wananena kwa lugha zingine

*Kamusi ya Merriam-Webster*: “Maneno ya usemi ambao hutoka kwa kasi kutoka ndani ya mtu na ambao huandamana na hisia nyinyi; usemi huu huiga lugha inayoeleweka, lakini wakati mwinge usemi wenyewe haueleweki na wasikilizaji wake; wakati mwinge usemi huo hunenwa katika hali za juu za hisia wanazohisi wale ambao wananena.”

## Xenoglossia (Zee-nuh-GLOSS-ee-uh)

Neno hili linatokana na maneno maawili ya Kiyunani: *xenos* (maanake mgeni) na *glossa*. Neno lenyewe linaashiria hali ambayo mtu anaweza kunena lugha ya ukweli (ya kigeni) ambayo kamwe hakuwahi kujifunza. Hii ni lugha ambayo inaweza kueleweka na mtu mwininge ambaye aijua lugha hiyo. Ni uneni ambao unaeleweka.

Ni muhimu mtu kuelewa maana ya neno “kunena kwa lugha nyininge” kama liliyotafsiriwa kutoka kwa nakala za mwanzo kabisa za lugha ya Kiyunani. Kuna mafundisho mengi ambayo yamezuka kutoptaka na watu kutoelewa lugha ya Biblia kama ilivyo kwenye tafsiri, na kutoptaka na watu kuchukua maandiko fulani bila kutazama muktadha wake. Kwenye kitabu cha Matendo ya Mitume na Wakorintho wa Kwanza kila wakati neno *glossa* linatumiwa kuzungumzia kunena kwa lugha nyininge neno hilo linadhihirisha maana kwamba lugha inayozungumzwa ni lugha ambayo inaweza kueleweka. Kwa kweli neno hilo halikuwahi kutumiwa kumaanisha matamshi ambayo hayawezi kueleweka ama kuguzia jinsi ambavyo neno *glossolalia* linatumiwa katika siku hizi zetu.

Katika siku hiyo ya Pentekoste watu wa Mungu walinena kwa lugha za kidunia kwa wageni hao kwa kutumia lugha za kidunia za wageni hao. Huu ndio mfano wa vile neno *xenoglossia* linavyotumiwa. Ni muhimu kuelewa kwamba tafsiri ya

neno “ndimi au lugha nyininge” linatokana na neno *dialektos* na *glossa* kwa kutumia lugha ya Kiyunani na maneno hayo yalitumika kwa njia ya mbadala (moja badala ya nyininge) kuonyesha kwamba wanafunzi hao walikuwa wakizungumzaa lugha zinazojulikana lakini ambazo zilikuwa tofauti na lugha zao za mama.

*Matendo 2:4 Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha [glossa] nyininge, kama Roho alivyowajalia kutamka*

*Matendo 2:6 Basi sauti hii ilioposikiwa makutano walikutanika, wakashikwa na fadhaa, kwa kuwa kila mmoja aliwasikia wakisema kwa lugha [dialektos] yake mwenyewe.*

*Matendo 2:8 Imekuwa je basi sisi kusikia kila mtu lugha [dialektos] yetu tuliozaliwa nayo?*

*Matendo 2:11 Wakrete na Waarabu; tunawasikia hawa wakisema kwa lugha [glossa] zetu matendo makuu ya Mungu.*

Kwa kusoma maandiko watu wanaweza kuelewa kipawa cha kunena kwa lugha nyininge kama kilivyo kuwa katika siku hiyo ya Pentekoste. Biblia inatoa maelezo mengi kuhusiana na kipawa hicho cha kunena kwa lugha nyininge—maana yake na matumizi yake. Hakuna mahali kwenye maandiko ambako kipawa hicho kinatumia kuonyesha mtu kunena maneno ambayo hayaeleweki huku yakiandamwa na hisia nyinyi moyoni, kama jinsi ambavyo jambo hilo linaonekana kwenye ulimwengu wa kisasa. Katika maandiko yaliyonukuliwa hapo juu kwenye Matendo ya Mitume “unenaji wa lugha nyininge” unaonekana kwa njia ambayo ni safi kabisa, na ambayo haijaingiliwa na uwongo na kwa hivyo huo ndio mfano ambao unalingana na jinsi ambavyo Mungu alitoa kipawa hicho kwa Wakristo.


# KUNENA KWA LUGHA NYINGINE

## BIBLIA NDIO MWONGOZO WETU

Matukio ya watu kunena au kuomba “kwa lugha nyingine” kwa furaha nyingi moyoni n.k. ni jambo ambalo limesambaa kati ya Wakristo na hata wasiokuwa Wakristo kote ulimwenguni. Jambo hili linasambaa katika madhehebu mbali mbali ya Kikristo na washirika wake wanadai kwamba ni jambo ambalo linalotokana na Roho Mtakatifu. Lakini tunahitaji kuzingatia kwamba Neno la Mungu ndilo mwongozo wetu na mafunzo na mazoea yote ya tabia zetu yanahitaji kulingana na Biblia—bila kujali maoni, ujuzi, na mambo mengine yanayoonekana kwa kimwili: “Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki” (2 Timotheo 3:16).

## KUWA MACHO DHIDI YA MAFUNDISHO YA UWONGO

Yesu alipatia kanisa onyo lifuatalo: “Kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule” (Mathayo 24:24). Shetani haji tu kwa kuonekana kama “mtu” mwovu bali pia huja kama malaika wa mwangaza na ambaye anatenda miujiza. Ni jambo muhimu kwamba watu wakumbatie ukweli na kukataa upotovu. Watu wengi huhadaliwa kwa mafundisho ya uwongo ya glossolalia, mafundisho ambayo yanäsambaa kote nchini. Jambo hili linawafanya washiriki wa unenaji kwa lugha nyingine kujihisi kwamba wako salama kwa mambo ya kiroho, na pia linadhoofisha nafasi ya watu kupata ujuzi wa kweli wa Roho Mtakatifu na kuweza kuishi maisha matakatifu. Lakini kunena kwa lugha nyingine ambako kunafanyika katika siku zetu hakutokani na Roho Mtakatifu bali hutokana na roho mbadala. Ni jambo muhimu kwamba kila mtoto wa Mungu aelewe ukweli wa “kunena kwa lugha nyingine” na atambue upotovu wa mengi ya mafundisho, mila, na tamaduni za kisasa kuhusiana na swala hilo.



## YALIYOTOKEA KATIKA SIKU YA PENTEKOSTE

*Wanafunzi walikuwa wakisema  
kwa uwazi kabisa na kwa  
Mpangilie wa lugha  
kwa kutumia lugha ya kigeni.*

ujuzi kama ule wa siku ya Pentekoste wa kuzungumza kwa lugha nyingine. Lakini kama jambo hilo lingekuwa kweli watu hawa wangkuwa wakizungumza lugha ya kiwanadamu kushuhudia nguvu za Mungu, badala ya kusema maneno ambayo hayaeleweki, maneno ambayo ndio yamejaa makanisa mengi siku hizi.

## KIPAWA CHA KUNENA KWA LUGHA LUGHA NYINGINE

Mtume Paulo anaelezea kuhusu wingi wa vipawa

(Inaendelea kutoka ukurasa 6)

## KUNENA KWA LUGHA MPY

Yesu aliwapatia wanafunzi wake wajibu wa kwenda kote ulimwenguni na kuihubiri injili: “Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha [glossa] mpya” (Marko 16:17). Andiko hilo ndilo la pekee katika Vitabu vya Injili ambako kunena kwa lugha kunasemwa kuwa ni kipawa ama ishara. Jambo hili lilitimika kwa kiwango kikubwa sana katika siku ya Pentekoste, wakati ambapo wanafunzi “...wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine” (Matendo 2:4) “kwa kuwa kila mmoja aliwasikia wakisema kwa lugha [dialektos] yake mwenyewe...” (Matendo 2:6).

Wanafunzi hao walikuwa wakinena kwa lugha “mpya” au kwa lugha “nyingine.” Kwa kweli hawakuwa wamejifunza lugha hiyo lakini waliweza kuizungumza kuititia kwa nguvu na kipawa cha Roho Mtakatifu.

Wanafunzi hao hawakuwa wakisema maneno yasiyo na maana au yasiyoleweka. Badala yake walikuwa wakisema kwa uwazi kabisa na kwa mpangilie wa lugha kwa kutumia lugha ya kigeni. Kwa nguvu za Roho wanafunzi hao walikuwa wakianzisha huduma kwa watu ambaa waliishi nje ya nchi ya Israeli na ambaa walizungumza lugha tofauti na wana wa Israeli.

Katika siku zetu watu wengi hudai kwamba wamebatizwa kwa Roho Mtakatifu na kwamba wamepata

ujuzi kama ule wa siku ya Pentekoste wa kuzungumza kwa lugha nyingine. Lakini kama jambo hilo lingekuwa kweli watu hawa wangkuwa wakizungumza lugha ya kiwanadamu kushuhudia nguvu za Mungu, badala ya kusema maneno ambayo hayaeleweki, maneno ambayo ndio yamejaa makanisa mengi siku hizi.

## KIPAWA CHA KUNENA KWA LUGHA LUGHA NYINGINE

Mtume Paulo anaelezea kuhusu wingi wa vipawa



vinavyotolewa na Roho Mtakatifu: "Basi pana tofauti za karama; bali Roho ni yeye yule" (1 Wakorintho 12:4). Roho Mtakatifu hawapatii watu wote kipawa kimoja: "Maana mtu mmoja kwa Roho apewa neno la hekima; na mwingine neno la maarifa...mwingine Imani...karama za kuponya...mwingine matendo ya miujiza; na mwingine unabii; na mwingine kupambanua roho; mwingine aina za lugha [*glossa*]; na mwingine tafsiri za lugha; lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye yule, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye" (1 Wakorintho 12:8-11).

Mungu hutoa vipawa vya Roho Mtakatifu kulingana na jinsi anavyoona zitafaidi mwili wa Kristo na kufaidi kazi ya Ufalme wa Mungu. Kipawa cha kunena kwa lugha nyingine kama kilivyokuwa katika siku ya Pentekoste ni uwezo wa mtu kuzungumza kwa lugha ya kigeni ambayo mtu hakujifunza lakini ambayo imetolewa kwa nguvu za Roho ili mtu huyo aweze kushiriki injili na watu wengine kwa ndimi au lugha zao. Neno *glossa* (au lugha) kama linavyotumika katika 1 Wakorintho ni neno lile lile ambalo linaonekana katika Matendo ya Mitume 2. Hiki sio kipawa cha kusema maneno yasioleweka ama kuzungumza lugha isijojulikana na wanadamu. Kipawa cha kunena kwa lugha zingine hakikuwa kipawa cha *glossolalia* bali kilikuwa ni kipawa cha *xenoglossia*.

#### KIPAWA CHA KUTAFSIRI LUGHA NYINGINE

Kipawa cha kutafsiri lugha zingine ni kipawa maalum cha Roho cha kutafsiria mtu ambaye

anazungumza lugha yake ambayo ni tofauti na lugha ya wasikilizaji wake. Kama katika siku ya Pentekoste wanafunzi hao hawakuwa na kipawa cha kunena kwa lugha nyingine basi wangehitaji mtu mwingine mwenye kipawa cha kutafsiri ili atafsiri ujumbe wao kwa lugha ya wasikilizaji wao. Lakini watu siku hizi wanasema maneno yasioleweka kwa furaha nyingi halafu wanadai kwamba wanahitaji kuwa na mtafsiri. Lakini jambo hilo liko mbali na kipawa cha kweli cha kunena kwa lugha nyingine, na hata liko mbali na kipawa cha kutafsiri lugha. Mahali ambapo kuna kipawa cha kunena kwa lugha nyingine hamna haja ya kuwa na mtafsiri kwani kila mmoja wa washirika ataaelewa kwa lugha yake ya mama.

#### LAKINI SIO WATU WOTE WAMEPEWA KIPAWA CHA KUNENA KWA LUGHA NYINGINE

Watu wengi humtafuta Mungu kwa bidii ili wapate kupewa kipawa cha kunena kwa lugha nyingine kwa sababu wao huonelea kipawa hicho ni spesheli sana, hata ingawa hawakielewi vizuri. Lakini mtume Paulo alisema katika 1 Wakorintho 12:31, "Takeni sana karama zilizo kuu. Hata hivyo nawaonyesha njia iliyobora." Kutoka hapo mtume huyo alielezea umuhimu wa upendo katika sura ya 14 ya kitabu hicho. Kama watu wangekuwa na shauku kubwa kuhusu upendo kama walivyo na shauku kuhusu kunena kwa lugha ulimwengu huu ungekuwa mahali tofauti kabisa. Hata ingawa sio kila mtu hupata kipawa kile kimoja kutoka kwa Roho Mtakatifu, kila mtu anaweza kumpokea Roho Mtakatifu mwenyewe.

#### MIFANO YA KIPAWA CHA KUNENA KWA LUGHA NYINGINE KATIKA BIBLIA

Isipokuwa siku ya Pentekoste kuna nyakati mbili zaidi ambako kwenye Biblia watu wamenukuliwa wakimpokea Roho Mtakatifu na kusema kwa lugha nyingine. Miaka michache baada ya siku hiyo ya Pentekoste Petro alihudumu nyumbani kwa Kornelio na Roho Mtakatifu akawashukia wote waliokuwemo: "Na wale waliotahiriwa, walioamini, wakashangaa...kwa sababu Mataifa nao wamemwagiwa kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa maana waliwasikia wakisema kwa lugha, na kumwadhimisha Mungu" (Matendo 10:45-46). Baadaye Petro akashuhudia na kusema "...Roho Mtakatifu akawashukia kama alivyotushukia sisi mwanzo" (Matendo 11:15). Zaidi ya hayo Roho Mtakatifu aliwashukia wanafunzi wa Yohana Mbatizaji huko Efeso ambao walimpokea Kristo. Wao pia "...wakaanza kunena kwa lugha [*glossa*], na kutabiri" (Matendo 19:6).

Roho Mtakatifu hakutolewa tu kwa Wakristo kupokea katika siku ya Pentekoste bali alitolewa kwa waumini wote ambao wangefungua miyo yao na kumtafuta Mungu ili wapate kujazwa. Katika nakala hizo mbili za ziada ambazo zimetajwa

katika Biblia Mungu pia alitoa kipawa cha kunena kwa lugha nyingine kama alivyofanya katika siku ya Pentekoste. Lakini pia kwenye nakala hizo waumini hawakuwa wakisema mambo yasioeleweka bali walikuwa wakisema kwa lugha za wasikilizaji wao. Kusema kwamba matukio hayo hayakuwa hivyo itakuwa ni upotovu wa kile ambacho Maandiko yamesema wazi wazi. Kwa kipawa hicho cha lugha za kigeni wanafunzi walitabiri au kufundisha mafundisho ya Kristo kwa kutumia lugha hizo za kigeni.

#### SIO KILA MTU HUZUNGUMZA KWA LUGHA NYINGINE

Makanisa mengi ambayo washiriki wake hunena kwa *glossolalia* (maanake kunena kwa lugha isioeleweka) hufundisha kwamba unenaji huo ndio ushahidi wa kuweko Roho Mtakatifu maishani mwa mtu. Lakini ni makosa kuamini hivyo, na pia ni makosa mtu kuamini kwamba kila Mkristo atapata ujuzi wa kweli wa kunena kwa lugha nyingine. Mungu ndiye huweka washirika mwilini mwa Kanisa lake na Yeye ndiye hugawa vipawa vya Roho kwa jinsi anavyotaka. Mtume Paulo aliuliza maswali ili kusisitiza jambo hilo katika 1 Wakorintho 12:28-30. "Je! Wote ni mitume?

Wote ni manabii? Wote ni waalimu? Wote wanatenda miujiza?" Jibu la maswali haya yote ni

"Hapana." Mtume Paulo akaendelea kuuliza, "Wote wana karama za kuponya wagonjwa? Wote wanena kwa lugha [kwa lugha za kigeni]? Wote wafasiri?" Na jibu ni lile lile: "Hapana."

#### KUNENA LUGHA (ZA KIGENI) NI MOJA TU YA VIPAWA VYA ROHO

Hata ingawa katika Matendo 2 baadhi ya wanafunzi 120 walinena kwa lugha za kigeni wengi wao ambao walimpokea Roho Mtakatifu hawakunena kwa lugha nyingine. Wakati watu wa Samaria waliposikia neno la Mungu na kuokoka Petro na Yohana waliwaombea na wakampeka Roho Mtakatifu (Matendo 8:14-17). Lakini wao hawakunena kwa lugha nyingine. Hata mtume Paulo hakunena kwa ugha nyingine wakati ambapo alimpokea Roho Mtakatifu. Hata Yesu pia hakunena kwa lugha nyingine wakati Roho Mtakatifu alimshukia.

Kunena kwa lugha za kigeni si jambo lilioamriwa, na wala si jambo ambalo lilifanywa na watu wote waliojazwa Roho Mtakatifu, na hata jambo hilo halikuonekana maishani mwa Kristo. Kunena kwa lugha ni kipawa kimoja tu cha Roho Mtakatifu ambacho kilitolewa kwa wakati uliohitajika ili kiwe ushuhuda kwa wasioamini (1 Wakorintho 14:22) na ndiposa Ijili isambae na watu waweze kuamini.

#### USHAHIDI WA KUWEKO ROHO MTAKATIFU NI NGUVU ZA MTU KUISHI MAISHA MATAKATIFU

Ushahidi wa kweli wa Roho Mtakatifu huonekana kwa mtu kuwa na uwezo wa kuishi maisha matakatifu na kuzaa tunda la Roho (Wagalatia 5:22-23). Ni kutokana na tunda hilo ndipo maisha ya kiroho ya mtu hujulikana kwa kweli. Kuna watu wengi ambao hutoa tu maneno ya "kunena kwa lugha" na kusema mambo yasiyoeleweka. Wao hudai kwamba wanaye Roho Mtakatifu lakini wangali wanaishi dhambini na wanaishi maisha ya kutotii Neno la Mungu. Kusema kweli wao hawajajazwa Roho Mtakatifu kwani Roho Mtakatifu anaweza tu kuishi kwenye hekalu safi na takatifu.



**Kunena kwa lugha za kigeni si jambo lilioamriwa, na wala si jambo ambalo lilifanywa na watu wote waliojazwa Roho Mtakatifu, na hata jambo hilo halikuonekana maishani mwa Kristo.**


#### TAMATI

Biblia imetoa mwongozo dhabiti wa siku ya Pentekoste ili watu waweze kuelewa kipawa cha kunena kwa lugha nyingine na kuonyesha kwamba lugha ambayo wanafunzi walinena nayo wakati huo ilikuwa ni lugha ya kibinadamu lakini iliyokuwa ya kigeni. Lakini madhehebu ya "kunena kwa lugha" yamepata mamilioni ya washirika ambao wanavutiwa na kitu kinachoonekana kuwa cha kiungu. Kama mtu anaweza kupata ujuzi huu na kuendelea kuishi dhambini atakuwa na shauku ipi ya kupata ujuzi wa kweli na wa kibiblia wa Roho Mtakatifu? Lakini kutoa tu maneno yasioeleweka na kusema kwamba mtu "ananena kwa lugha" si jambo ambalo linalotokana na Roho Mtakatifu bali linatokana na roho ya kuwahadaa Wakristo na ambayo ni kinyume chake Roho wa Mungu. Mungu hataki kuabudiwa kwa njia ambazo si halali. Uwepo wa Roho Mtakatifu hauonekani kwa mambo ya mtu kujionyesha bali huonekana kwa mtu kuishi maisha ya utakatifu, amani, na furaha.

—mws

# Lugha ya Maombi

## "Lugha ya Malaika"



Kuna mafundisho mengine ya uwongo ambayo yamekaribiana sana na mazoea ya watu kunena lugha sisizoleweka. Haya ni mazoea ya watu kuomba kwa lugha zingine kwa kile ambacho kinajulikana kama "lugha ya maombi" au "lugha za malaika." Kuna wale ambao hutumia lugha hizi hadharani na wengine hufundisha kwamba "hii ni lugha ya maombi ya kibinagsi." Wakati watu wanaomba kwa njia hii wao huwa wanazungumza maneno na kutoa sauti ambazo hazina maana yoyote kwao wala kwa wasikilizaji wao.

Lakini ukweli haupimwi kwa mazoea ya watu bali hupimwa kwa kutumia Neno la Mungu. Mambo haya yakipimwa kwa mizani ya maandiko inagunduliwa kwamba (haya) ni mafundisho mapotovu ya wanadamu na sio mafundisho yanayotokana na Mungu—kwa maana kamwe hayakubaliani na Maandiko yake.

### TUMEPEWA MWONGOZO WA JINSI YA KUFANYA MAOMBI

Tumefundishwa kuomba "...katika Roho Mtakatifu" (Yuda 1:20) na kuomba kila wakati "...kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho" (Waefeso 6:18). Roho Mtakatifu ndiye ambaye hutuongoza na kutupatia mwelekeo na hata kutusaidia ili tujue jinsi ya kuomba kulingana na mapenzi ya Mungu. Basi tunahitaji kuomba kwa uwazi kama watu wakweli kwa Mungu, huku tukiishi maisha ya utakatifu na kuomba kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu.

### ROHO MTAKATIFU ANATUOMBEA

Watu wengine hunukuu Warumi 8:26b inayosema kwamba "... Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa." Lakini andiko hilo liko kinyume na mafundisho ya watu wanaosema kuna lugha ya maombi, ambao wanalitumia kuegemeza

mafundisho hayo. Andiko lenyewe linasema Roho "hutuombea" na halisemi kwamba Roho huyo "ataomba" kutoka ndani mwetu. Pia andiko lenyewe linasema kuugua huko kwa Roho "hakuwezi kutamkwa" maanake hakuwezi kunenwa. Ukweli unaofundishwa na andiko hilo ni kwamba, Roho wa Mungu hutusaidia na kutuhudumia ili tuweze kubeba mizigo ambayo huuguza hisia zetu kindani maishani mwetu.

### UGHA ZA WANADAMU NA ZA MALAIKA

Kuna watu wengi ambao hutumia mafundisho ya Mtume Paulo katika 1 Wakorintho 13:1 kuunga mkono swala la watu kunena au komba kwa lugha ya malaika: "Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika." Neno "nijaposema" limetokana na neno la Kiyunani *ean* ambalo linaashiria kutokuwa na uhakika wa



Malaika...hawakusema  
maneno yasiyo na maana...  
bali walizungumza 'lugha ya mama'  
ya msikilizaji wao.

jambo. Tafsiri ambayo ingefaa zaidi ni kutumia neno "kama." "Kama ningesema kwa lugha za wanadamu na za malaika . . ." Kusema kweli mtume Paulo hakuzungumza lugha zote za wanadamu na pia hakuzungumza lugha za malaika. Yeye hakufanya milima indoke na hakutoa mwili wake kuchomwa. Hapa mtume Paulo alikuwa tu anatilia mkazo wazo ambalo lilitegemea lile lingine ili kuonyesha jinsi upendo ulivyo mkuu zaidi.

Watu wanahitaji kuelewa “Lugha za malaika” *kama* uwezo kwa ufasaha na kwa ukamilifu. Kama watu wangalikuwa na uwezo wa kuomba au kunena kwa lugha za malaika basi ingalikuwa ni jambo la busara kwetu kuchunguza jinsi malaika walivyzungumza hapa duniani. Malaika alisema na Zakaria (Luka 1:13), akasema pia na wachunga kondoo (Luka 2:10), akasema na Petro (Matendo 12:8) na kadhalika. Malaika hao ambao walikuwa wajumbe wa kiungu hawakusema maneno yasiyo na maana au yasioleweka bali walizungumza ‘lugha ya mama’ ya msikilizaji wao.

Wakorintho wa Kwanza 13:8 inaendelea kusema: “Upendo haupungui neno wakati wo wote; bali ukiwapo unabii utabatiliaka; zikiwapo lugha, zitakoma; yakiwapo maarifa, yatabatiliaka. Kwa maana tunafahamu kwa sehemu; na tunafanya unabii kwa sehemu.” Kama lugha nyiningine (ya kigeni) ingalikuwa ya kimalaika basi ingekomaje? Je, malaika hao wängeshindwa kunena? Hakuna jambo ambalo mtume Paulo alisema ambalo lilionyesha kwamba ye ye alizungumza kwa lugha ya malaika, na maandiko kamwe hayaungi mkono dhana kwamba kuna kitu kama hicho.



#### **NENO “ISIYOJULIKANA” LIMEONGEZEWА KATIKA TAFSIRI ZINGINE**

Watu wa madhehebu ya Kipentekoste ambao hufundisha kwamba kuna lugha ya “maombi ya siri” hutumia 1 Wakorintho 14:14 kuendeleza msimamo huo: “Maana nikiomba kwa lugha [glossa] (watafsiri wengine wameongeza neno “isiyojulikana”), roho yangu huomba, lakini akili zangu hazina matunda.” Neno glossa ndilo ambalo limetumika hapo, na ambalo maana yake ni lugha ya kigeni, wala sio mtu kusema maneno yasiyooleweka. Basi mtu akitafsiri neno glossa na kulipatia maana ya mtu kusema au kuomba kwa maneno yasiyooleweka atakuwa akitafsiri biblia kwa njia ambayo si halali.

Je, mtu akiomba kwa lugha ya kigeni atakosa kuzaa matunda kwa nani? Kwa kweli yeye atakosa kuzaa matunda kwa msikilizaji wake kwa maana msikilizaji huyo hataelewa lugha hiyo ikiwa kwamba lugha hiyo si yake ya kuzaliwa. Je, mtu akiomba na lugha ya kigeni “... yeye akekiye katika mahali pa mjinga ataitikaje, Amina, baada ya kushukuru kwako, akiwa hayajui usemayo?” (1 Wakorintho 14:16).

Mtume Paulo amesema kwamba “mjinga” au asiye na elimu hataweza kuelewa maombi hayo; sio eti kwamba maneno ambayo yanatoka kwa mtu anayeomba hayana maana yoyote,

bali kwamba msikilizaji hajasomea au kusomeshwa lugha hiyo ya kigeni. Yule ambaye amesoma au kujifunza lugha hiyo ataelewa maombi hayo. Lakini maombi yenewe hayatakuwa na matunda yoyote na pia hayatamjenga yeyote ambaye kamwe hajui kunena lugha hiyo.

#### **YESU AMETOА MWONGOZO KWAMBA WAKRISTO WASIJIRUDIE RUDIE KWENYE MAOMBI**

Bila kuzingatia mafundisho ya wanadamu hebu wewe tazama mfano wa Yesu alipokuwa akifundisha jinsi ambavyo wafuasi wake wanahitaji kuomba. Mathayo 6:7-13 inasema: “Nanyi mkiwa katika kusali, msipayuke-payuke (kujirudia-rudia), kama watu wa mataifa” (7). Neno la Kiyunani la kupayuka ama kujirudia-rudia ni mtu kuongea kwa kusitasita. Basi ni dhahiri kwamba tunahitaji kuomba kwa uwazi na kwa urahisi. Watu wa mataifa na waabudu sanamu watapayuka-payuka maneno maombini na kurudia maneno yale yale tena na tena. Lakini

*Nanyi mkiwa katika kusali,  
msipayuke-payuke, kama watu  
wa mataifa.  
Mathayo 6:7-13*

Yesu alisema tusifanye hivyo. Lakini hivyo ndivyo ambavyo wengi wa “wanaosema kwa lugha nyiningine” hufanya. Wao hufunza washirika wake jinsi ya kuomba kwa kurudia maneno yale yale tena na tena, jambo ambalo ni kinyume kabisa na mafundisho ya Neno la Mungu.

Katika mstari wa 9 Yesu anasema, “Bali wewe usalipo...” Yesu hakutoa makelele ya kigeni au kunena lugha isiyooleweka. Yeye aliomba kwa njia ya uwazi ambayo ilikuwa rahisi kuielewa. Kwa kweli ikiwa Mungu alitaka watu wake kuomba kwa lugha isiyojulikana Kristo angetufunza vingine; nasi twajua kwamba Kristo na Baba yake hawapingani, wao ni wamoja.

#### **USINDANGANYIKE NA MAFUNDISHO YA UONGO YA WANADAMU WENZAKO**

Katika Biblia hakuna ushahidi au mfano wa maombi wa kutumia lugha ya malaika. Kwa kweli jambo hilo ni upotovu wa ukweli na halitokani na Mungu. Wewe usitekwe na mafundisho na imani za mwanadamu. Unahitaji kufuata tu mfano wa Kristo ili atakaporudi awe na amani nawe.

—mws

# I WAKORINTHO 14

Katika nyakati za kisasa ndipo Wakristo wameanza kuchunguza maandiko ili kujihakikishia kwamba usemajii wao wa maneno yasiyokuwa na maana ambayo huandamana na furaha nyingi ni jambo ambalo linafaa. Lakini Kristo hakuanzisha jambo hilo bali lilikuwa ni mazoea ya watu wasiomjua Mungu. Basi tendo hili ambalo mizizi yake ni ukafiri na ambalo sasa linafanyika kanisani – pengine linatokana na hisia za mtu binafsi au huenda linatokana na roho wa uwongo. Kimakosa maneno hayo ya furaha inayotokana na kunena kwa aina hiyo huchukuliwa kwamba ni jambo la kiroho na la kiungu. Lakini usemi wa maneno na maombi kwa kutumia maneno yasiyoleweka halikuweko katika kanisa la kwanza na pia halipatikani katika kanisa la Mungu katika siku hizi zetu.

Hali ya kuchanganyikiwa kwa kiwango kikubwa na pia mafundisho ya uwongo yameanza kutokana na matumizi mabaya ya 1 Wakorintho 14, sura ambayo Mtume Paulo alishughulikia swala la kunena kwa lugha kwa mapana na marefu. Lakini kuchanganyikiwa huku hakutokani na Biblia bali kumetokana na wanadamu. Siku hiyo ya Pentekoste Mungu alionyesha kinaga ubaga kile ambacho kunena kwa lugha nyingine kilitakiwa kiwe. Neno *glossa* (lugha ya kigeni) ambalo limetumiwa katika Matendo 2 ndilo pia linatumwiwa katika 1 Wakorintho 14. Basi kwa kufuata mfano wa siku ya Pentekoste si jambo ngumu mtu kuelewa mafundisho ya Paulo kwa kanisa la Korintho.

Korintho ulikuwa mji mkubwa wa kilindini ambao ulijaa watu kutoka tamaduni na nchi mbali mbali. Kulikuwa na shida nyingi katika kanisa la Korintho ndiposa mtume Paulo akawaambia kwa njia ya moja kwa moja kwenye 1 Wakorintho 3:3, “Ninyi ni watu wa tabia ya mwilini....” Kitabu cha 1 Wakorintho hasa ni kitabu cha kukemea na kurekebisha kusanyiko ambalo lilikuwa ni la kimwili na ambalo halikuwa likifuata mafunzo ya jinsi Mkristo anastahili kuishi.



**“Paulo hakuwa akifundisha mafundisho mapya kuhusu kunena kwa lugha nyingine bali alikuwa akiwakemea kwa kukipatia kipawa hicho cha kunena kwa lugha za kigeni hadhi kubwa zaidi na kwa kukitumia vibaya.”**

Uchunguzi wa makini wa sura ya 14 unadhihirisha kwamba mtume Paulo hakuwa akifundisha mafundisho mapya kuhusu kunena kwa lugha nyingine bali alikuwa akiwakemea Wakorintho kwa kukipatia kipawa hicho cha kunena kwa lugha za kigeni hadhi kubwa zaidi na kwa kukitumia vibaya. Kusanyiko hilo lilikuwa katika hali ya fujo na kukosa utaratibu. Hata ingawa kulikuwa na uwezekano kwamba katika kusanyiko hilo kulikuwa na mtu ambaye alikuwa na kipawa cha kweli cha kunena kwa lugha, na ambaye aliweza kunena kwa lugha ambayo hakuwahi kujifunza; lakini huenda kwamba mambo hayakuwa hivyo, kwa maana Mungu hawesi kuwa chanzo cha kuleta hali ya kuchangayikiwa. Pengine ukweli ulikuwa kwamba kuna watu amba walikuwa wakijua lugha za kigeni na amba walikuwa wakizzungumza kwa njia ambayo haikujenga wasikilizaji wake amba walikuwa hawakuelewa lugha hiyo ya kigeni. Huenda watu hao hawakuwa na kipawa cha kweli cha kunena kwa lugha kwa maana kipawa hicho hutolewa kwa njia ya kiungu. Ndiposa Paulo akawapatia mwongozo kwamba walihitaji kumtafuta Mungu ili wapate kipawa cha utabiri (kuhubiri) ili kanisa liweze kujengeka. Ujumbe wa Mungu amba walihitaji utakuwa wa manufaa zaidi kuliko mtu kujionyesha kwamba anaweza kuzungumza kwa lugha ya kigeni, lakini kwa njia ya kiburi.

Hebu basi tutazame mistari kadhaa katika 1 Wakorintho 14 na maana yake—huku tukizingatia kwa njia ya uwazi kabisa kwamba maana ya kunena kwa lugha nyingine ni kunena lugha ya kigeni. (Zingatia kwamba: Katika lugha ya Kiingereza ya KJV neno “isiyojulikana” liliongezewa na watafsiri. Neno hilo halikuweko katika nakala za mwanzo na ndiposa neno hilo haliko kwenye tafsiri nyingi za baadaye.)

**(Mustari wa 2) Maana yeye anenaye kwa lugha, hasemi na watu, bali husema na Mungu; maana hakuna asikiaye; lakini anena mambo ya siri katika roho yake.**

Yule anenaye siri za Mungu kwa lugha ya kigeni haneni na wanadamu bali hunena na Mungu ikiwa hakuna mtu hapo ambaye anaelewa lugha hiyo ya kigeni. Katika mistari wa 2-3 Mtume Paulo anatilia mkazo umuhimu wa kuhubiri kama njia ya kujenga kanisa. Yule ambaye anasema kwa lugha ya kigeni anajijenga yeye mwenyewe kwani yeye peke yake ndiye aelewaye kile anachosema.

**(5) Nami nataka ninyi nyote mnene kwa lugha, lakini zaidi sana mpate kutoa unabii, maana yeye atoaye unabii ni mkuu kuliko yeye anenaye kwa lugha, isipokuwa afasiri, ili kusudi kanisa lipate kujengwa. (6) Ila sasa, ndugu, nikija kwenu na kunena kwa lugha,**

**nitawafaidi nini, isipokuwa nasema nanyi kwa njia ya ufunuo, au kwa njia ya elimu, au kwa njia ya hotuba, au kwa njia ya fundisho? (tazama pia mstari wa 12-13).**

Mtume Paulo angefurahi kama watu wote wangenena kwa lugha tofauti lakini akawaambia watafute vipawa ambavyo vingejenga kanisa (na sio lugha ya kigeni ambayo hufanya watu kuchanganyikiwa). Lakini kutoa unabii ni kipawa kikuu zaidi iwapo hakuna mtu ambaye anaweza kufasiri lugha ya kigeni ambayo mnenaji ananena ili kanisa lote lipate kujengwa. Je, Paulo atapata faida gani kunena kwa lugha nyiningine ikiwa hakuna mtu atamwelewa?

**(9) Vivyo hivyo na ninyi, msipotoa kwa ulimi neno lililo dhahiri, neno lile linenwalo litajulikanaje? Maana mtakuwa mkinena hewani tu. (10) Hakika ziko sauti za namna nyangi duniani, wala hakuna moja isiyo na maana. (11) Basi nisipojua maana ya ile sauti nitakuwa kama mjinga kwake yeze anenaye; naye anenaye atakuwa mjinga kwangu.**

Haijalishi mtu anayenena ana ukweli gani, ikiwa wale ambao anawanenea hawaelewii lugha anayozungumza maneno yake yatapotea bure na wasikilizaji wake hawatamwelewa. Kuna lugha nyangi za kigeni ulimwenguni na zote huwa na maana. Lakini ikiwa wewe huelewii lugha hiyo basi sauti zake husikika kama za kishenzi au za kigeni. Ni dhahiri kwamba mtume Paulo hapa hazungumzii lugha ambayo haiwezi kueleweka.

**(Kwa mistari ya 14-17 tazama “Lugha ya Maombi” katika ukurasa wa 9).**

**(22) Basi, hizi lugha ni ishara, si kwao waaminio, bali kwao wasioamini lakini kutoa unabii si kwa ajili yao wasioamini, bali kwa ajili yao waaminio. (23) Haya! Ikiwa kanisa lote limekusanyika pamoja, na wote wanene kwa lugha, kisha ikawa wameingia watu wajinga au wasioamini, je! Hawatasema ya kwamba mna wazimu? (24) Lakini wote wakitoa unabii, kisha akaingia mtu asiyeamini, au mjinga, adhihirishwa na wote, ahukumiwa na wote:**

Kusudi kuu la kipawa cha kunena kwa lugha ya kigeni ni kwamba iwe ishara kwa mtu asiyeamini ili aweze kuisikia injili na apate kuokolewa kama siku hiyo ya Pentekoste. Lakini ikiwa kila mtu atakuwa akizungumza kwa lugha tofauti, aidha kwa kutumia kipawa au kwa kujifunza, na iwe kwamba wajinga (wale ambao hawaelewii lugha hiyio) au wasioamini waje huko, watafikiri nyote ni wenye kichaa kwa ajili ya fujo ya lugha ambayo mmezusha. Lakini ni bora zaidi mtu kuhubiri kwa lugha ya mama ya mtu yule asiyeamini ili aweze kuelewa na apate kuokolewa.

**Katika mistari ya 26-28 mtume Paulo anaendelea kusema kuhusu fujo ya kunena kwa lugha ambayo haijengi na akatoa mwongozo kwamba: ikiwa utanena kwa lugha ya kigeni hakikisha kwamba kuna wale ambao wanaelewa lugha hiyo. Lakini kama hakuna mfasiri basi wewe nyamaza kanisani na uzungumze na Mungu wako.**

Ikiwa mtu ataelewa kwamba matumizi bora ya “lugha nyiningine” ni kuwanenea wasioamini kwa lugha yao wenyewe ili wajengeke ni jambo ambalo litaleta mwanga katika hali ya kuchanganyikiwa ambayo imeingizwa katika sura hii ya 1 Wakorintho 14. Glossa ilikuwa (na hata sasa ingali) lugha ya kigeni na haijawahi kuwa lugha isiyo na maana. Basi mtume Paulo akamalizia kwa kuliambia kusanyiko la Korintho kwamba kunena kwa lugha ya kigeni si jambo ambalo limekatazwa lakini ni jambo ambalo linahitaji kuweko na mtu wa kutafsiri: “Lakini mambo yote na yatendeke kwa uzuri na kwa utaratibu” (1 Wakorintho 14:40). —mws



**Je, ikiwa mimi nishawahi kusema kwa lugha  
kwa kutumia maneno yasiyo na maana  
hii ni kusema kwamba sijaokoka?  
Je, ninastahili kufanya nini?**

Sio laana ikiwa mwangaza wa ukweli utaangazia maisha yetu. Jambo lililo halisi ni kwamba tunapokubaliana na ukweli sisi hutata uhuru mwingu zaidi na ushindi ndani yake Roho Mtakatifu. Kama ilivyo kweli kuhusiana na mafundisho mengine ya uwongo, kunawenza kuwa na watu wengi wasio na makosa ambao hujipata wameingiana na uongo kwa kukosa kujua Neno la Mungu. Adui yetu ana hadaa nyangi na amefaulu kushika watu wengi kwa njia hii yake ya kuingiza uongo kuhusu swala la kusema kwa lugha nyiningine.

Hebu basi yachunguze maisha yako mbele zake Bwana. Je, wewe unaishi maisha yasiyo na dhambi, ama unaendelea kufanya matendo ya kimwili? Kama kuna dhambi maishani mwake unahitaji kutubu. Kama pia una mazoea ya kufanya glossolalia, ama unayo lugha ya maombi ya kibinagsi, unahitaji kumtafuta Mungu mara moja ili akukomboe. Lakini huku si kusema kwamba jambo hilo limehesabiwa kuwa dhambi kwako kama wewe huujui ukweli; lakini kujua ukweli ni mtu kuwajibika. Ole wao waachao mwangaza ili kufuatilia mambo hayo yasiyo na uungu ndani yake.

Hii ndiyo sababu unahitaji kumuomba Mungu ili akusamehe na akupatie uhuru kamili kutokana na hisia au roho ambayo imekufanya kuwa na tabia kama hizo. Mungu atakusamehe na kukomboa kutokana na roho yoyote ya kigeni. Maombi ya pamoja huwa na nguvu sana na ingekuwa jambo ambalo linafaa ikiwa utamruhusi mtu mwagine kuomba nawe ili ukombolewe kikamilifu kutokana na roho au lugha hiyo ya kigeni isiyo ya ukweli.

Pia litakuwa jambo la busara ikiwa utaacha mara moja kuabudu na watu ambao wanafundisha na kunena kwa lugha sisizo na maana ili wasikuadhire. Unahitaji kutafuta ushirika mpya na watu wengine watauwa ambao wanaishi katika utakatifu wa kweli.

Ni ombi langu kwamba Mungu atakupatia hekima, na pia kwamba atakupatia ukombozi wa kiungu kupitia kwa damu yake Yesu Kristo na kwa nguvu za Roho Mtakatifu. Amina.

—mws



**JE, WAJUA?**

Mazoea ya watu kunena kwa lugha nyingine ambazo huwaletea furaha na ambazo pia hufasiriwa ni kitu ambacho kilikuweko hata kabla ya siku ya Pentekoste na chanzo chake si Ukristo. Jambo hili lilikuwa la kawaida katika dini za kale za kipagani na hata za kisasa, na zinafanana sana na usemajji wa maneno yasiyo na maana ambao unafanyika katika makanisa mengi ya kipentekote katika siku zetu.

Mazoea ya kunena kwa njia hii kunapatikana katika dini na nchi tofauti ulimwenguni kote. Ni jambo ambalo linapatikana kati ya Wakatoliki, watawuwa wa dini ya Buddha,

Washamani kutoka Ethiopia na hata kati ya Wahiti wanaoshiriki voodoo. Pia ni jambo linalotendeka katika makusanyiko yanayotafuta uwezo wa kuwasiliana naa mapepo ambayo hupatikana huko Japani, na pia kati ya dini za kitamaduni za makabila ya Kiafrika – na kati ya dini nyingi zaidi.




Neno  
Linalofaa kwa  
Msimu Huu

## Tweka Mpaka Kilindini

### Anwani

The Gospel Truth  
P. O. Box 2042  
Nixa, MO 65714  
USA  
Email:  
[editor@thegospeltruth.org](mailto:editor@thegospeltruth.org)

### UTAKATIFU KWA BWANA



*"Tweka mpaka kilindini, mkashushe nyavu zenu mvue samaki."* Luka 5:4

Wanafunzi wa Yesu walikuwa wamekazana usiku kuchwa kuvua samaki. Lakini wavuvi hawa wenye ustadi mkubwa hawakufaulu kuvua samaki yeyote. Ndiposa Yesu akawaambia ku- “TWEKA MPAKA kilindini...mkashushe nyavu zenu mvue samaki.”

Wakati mwangi tunavua samaki ‘wa kibinadamu’ na kumfanya Bwana kazi katika mahali petu padogo kama watu wale wengine. Pengine hapo ndipo mahali unajisikia kwamba u-shwari kabisa lakini baraka za mahali hapo zaweza kuwa ni ndogo sana na iwe kwamba hata idadi ya samaki unaowavua ni haba sana. Inawezekana mtu kuanza kurudi nyuma katika huduma yake kama ilivyokuwa kwa wanafunzi hao.

Wakati Yesu anapokuongoza kwa neno lake kwako wewe usiogope kuondoka kwa imani. Badala yake enenda katika sehemu mpya ya huduma ambako watu wanahitaji injili. Hebu msifu Mungu katika nyakati ambako hapo mbeleni ulikuwa ukikaa kimya. Hebu watumikie watu wale wengine wakati ambapo hapo mbeleni ulikuwa ukishughulika tu na matatizo yako ya kibinafsi. Mabadiliko hayo yanaweza kuwa madogo au makubwa, lililo muhimu ni wewe kumtii Bwana.

Kuna samaki ambao hawavuliki na kazi ambayo haitafanyika. Tunaweza kuzungumza kuhusu swala hili na kuliombea lakini samaki hao hawatavulika hadi hapo tutakapotweka nyavu zetu mpaka kilindini na kushusha nyavu zetu. Hebu tuache kumwekea Mungu mipaka na badala yake tuenende kulingana na mapenzi yake. Matokeo ya jambo hilo (la kuachia Mungu matokeo) huwa ni baraka kubwa zaidi, mtu kupata nguvu mpya, kupakwa mafuta upya, utukufu, na hata watu kuokoka.

Basi wewe mfanyi kazi mwenzangu, ninakuomba ushushe nyavu zako ili upate mvuo mkubwa wa samaki.

—mws